



BARAZA LA TAIFA LA WATU WANAOSHI NA VIRUSI VYA UKIMWI (NACOPHA)

TAARIFA YA KUFANYIKA MKUTANO MKUU WA BARAZA

Kwa mujibu wa Katiba ya Baraza sura ya Sita Kifungu 6.1. kinaelekeza Baraza kuwa kutakuwa na Mkutano Mkuu wa Baraza utakaoandaliwa na kuitishwa na Bodi ya Uongozi.

Kwa kuzingatia kifungu 6.1(iv), kwa niaba ya Bodi ya Uongozi wa Baraza napenda kutoa taarifa rasmi ya kufanyika mkutano Mkuu wa Baraza. Mkutano huu unatarajiwa kufanyika tarehe 25 na 26 October, 2018 kama ilivyoelekezwa na Bodi katika kikao chake cha kawaida tarehe 12/07/2018. Mkutano huu pia utahusika na uchaguzi mkuu wa Viongozi wa Baraza. Agenda zote za mkutano kwa wajumbe zitatolewa hapo baadae.

Kwa mujibu wa kifungu kidogo 6.1(ii) Wajumbe wa mkutano huu ni pamoja na wajumbe wote wa Bodi walioko madarakani, wawakilishi wawili kutoka kila mtandao wa kitaifa wa WAVIU, Wenyeviti wa Konga na mwakilishi mmoja kutoka kila kongu. Ikiwa mwenyekiti atakuwa mwanume, basi mwakilishi atakuwa mwanamake, au kinyume chake.

Kwa vile gharama za kuendesha mkutano mkuu ni kubwa sana, na uwezo wa Baraza kuwa mdogo, wajumbe wanaombwa kuchangia gharama za ushiriki kama vile usafiri au posho ya kujikimu. Tunaomba viongozi wote wa kongu waweze kushirikisha uongozi wa Halmashauri husika na wadau wengine ili waweze kupatiwa msaada pale inapowezekana.

Tunawatakia maandalizi mema.

Imetolewa leo tarehe 24/7/2018

Deogratius Peter Rutatwa
Afisa Mtendaji Mkuu
NACOPHA